

Maswali

1. Baba wa Mikali alikuwa nani?
2. Sauli alitaka Daudi afanye nini ili amuoet Mikali?
3. Daudi aliuwa Wafilisti wangapi?
4. Mikali alifanya Daudi nini ili asiuwawe na Sauli?
5. Kwa jamii ya Sauli nani mwingine alisaidia Daudi na wakawa marafiki?
6. Mbona Daudi alipompata Sauli hakumuua?
7. Daudi alileta nini Yerusalem?
8. Mikali alipomshambulia Daudi kwa kumchezea Mungu, Daudi alijibu nini?
9. Kwa ajili ya uovu wake, Mikali alipata watoto?

Majibu

1. Mfalme Sauli.
2. Alikuwa auwe Wafilisti 100.
3. Aliuwa Wafilisti 200.
4. Alimuonya juu ya mpango wa Sauli na akamsaidia kutoroka kupitia dirishani.
5. Yonathani naye alimsaidia Daudi na akawa rafiki wake mzuri.
6. Kwa sababu alimwogopa Mungu na aliamini kwamba atakuwa naye kwa hali yote.
7. Sanduku.
8. Daudi alijibu kwamba hakujali mazungumzo ya mtu yeyote kwa sababu alicheza mbele ya Mungu sio watu.
9. La hasha, hakupata watoto kwa sababu ya uovu wake kwa Daudi na hakumheshimu Mungu.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 2



17 Daudi na Mikali

Marejeo

- 1 Samweli 18, 19
- 2 Samweli 6

Kiini cha somo

Tukimpenda na tumuamini Mungu atatulinda

Maneno maalum

1. Mikali + alewa kwa Daudi + ua Wafilisti 100 + Daudi aliuua 200 + Daudi alioa Mikali.
2. Sauli aogopa + ua Daudi.
3. Yonathani + rafiki + Daudi + Kinubi + Sauli + mkuki.
4. Onyo ya Mikali + Daudi ahepa.
5. Sanamu (mfano) + watu wa Sauli.
6. Daudi amechificha + tii amri za Mungu + Paltiel.
7. Daudi akamchukua Mikali + akawa mfalme.
8. Sanduku + Yerusalem + Daudi anacheza + Mikali + anamdhara + tasa.

17.1 Mikali alikuwa bintiye mdogo wa mfalme Sauli. Mikali alimpenda Daudi na Sauli aliposikia akawaza, "Nitamtega Daudi kwa kumkubali aoe Mikali". Sauli alimwambia Daudi, "Umuoe binti wangu Mikali lakini kwanza uue Wafilsti 100." Hakutazamia kwamba Daudi atafanya hilo. Alishangaa kuona Daudi amerudi na ameuua Wafilsti 200, kwa hivyo akamkubali Mikali amuoee Daudi.

17.2 Sauli alipogundua kwamba Mungu alikuwa na Daudi, alimwogopa zaidi. Hapo Daudi na Sauli wakawa maadui na Sauli akapanga kumuua Daudi.



kwa mkuki. Daudi alihepa na mkuki ukagonga ukuta. Daudi alitoroka, usiku huo alipopata habari kwamba Sauli alinuwia kumuua kesho asubuhi.

17.4 Mke wake Mikali alimhadharisha, "Unatakiwa utoroke usiku huu, la sivyo utakufa asubuhi." Kwa hivyo Mikali alimteremshia dirishani naye akatoroka na kuenda.




17.3 Sauli alimwambia mwanawe Yonathani amuuue Daudi lakini Yonathani alikuwa rafiki wa Daudi kwa hivyo akamuonya. Yonathani alijaribu kumwambia Sauli kwamba Daudi alikuwa mtu mzuri lakini hakumusikiliza. Wakati fulani Daudi alipokuwa akimchezea kinubi, Sauli alitaka kumuua

17.5 Halafu Mikali akaweka sanamu kitandani iliyoonekana kama Daudi yuko ndani. Watu wa Sauli walipokuja, Mikali akawambia kwamba Daudi ni mgonjwa, wakagundua alikuwa amewadanganya. Wakauliza Mikali mbona alifanya hivyo. Akawaambia, "Kama singemsaidia Daudi angeuwawa."

17.6 Wakati mwingi Daudi alijificha ili watu wa Sauli wasimuue. Mda huo wote, Daudi alikuwa akipata nafasi ya kumuua Sauli. Hakufanya hivyo kwa sababu Daudi alimpenda Mungu na alitii amri zake. Daudi alioa wake wengine ingawaje Mikali alikuwa wake pia. Sauli alimuza kwa mtu mwingine aliyeitwa paltiel.

17.7 Baadaye Sauli alikufa lakini Daudi hakufurahia. Mungu akamwambia Daudi aende Hebron. Alipokuwa huko akataka mke wake Mikali aletwe, kwa hivyo akatuma wajumbe wamlete. Daudi akawa mfalme wa Israeli na akashinda Wafilsti.



17.8 Daudi alileta sanduku la Mungu Yerusalem. Alifurahi na akamchezea Mungu kwa sababu sanduku l i l i r u d i s h w a Yerusalem. Mikali alimwangalia kwa dirisha. Alimlaumu Daudi, alimfanyia msaha kwa ajili ya kucheza mbele ya watumwa mpaka nguo zikaanguka. Daudi alimwambia, "Nilichokifanya, nilifanya mbele ya Mungu aliyenichagua. Siwezi kuaibishwa mbele ya watumwa wangu, badala yake wataniheshimu zaidi." Kwa ajili ya hayo madharau, Mungu alimzuia kupata watoto maishani mwake.